**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**634** **STADI ZA KAZI**

**Muda: Saa 3.** **Mwaka: 2006**

**Maelekezo.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu **B** na **C.**
3. Sehemu A ina alama 40, sehemu B na C zina alama 30 kila moja.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Taja aina nne za ala za muziki kulingana na jinsi zinavyopigwa.
2. Bainisha madhara manne ya upungufu wa virutubisho muhimu mwilini.
3. Fafanua faida mbili za mwalimu kuandaa muhtasari wake wa somo.
4. Orodhesha vifaa vinne vya kusafishia na kung'arisha fanicha za nyumbani.
5. Eleza sababu nne za kufanya utafiti wa soko kabla ya kuanzisha biashara.
6. Taja aina nne za mistari inayotumika kuchora michoro ya vitambaa.
7. Bainisha malighafi nne za asili zinazotumika kutengeneza rangi za kuchorea.
8. Eleza matumizi mawili ya sindano ya mashine ya kushona.
9. Taja aina nne za samaki zinazofaa kufugwa katika madimbwi.
10. Orodhesha faida nne za kufuata kanuni za ushonaji.

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

11. Chambua vigezo sita ambavyo mwalimu anapaswa kuzingatia katika kuchagua mbinu za kufundishia.
12. Eleza kanuni tano za ufugaji wa nyuki kama mradi wa Stadi za Kazi.
13. Fafanua manufaa sita ya muziki katika maisha ya kila siku.
14. Changanua sababu sita za kuweka hifadhi ya akiba katika biashara ndogo.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

15. Eleza hatua sita za utunzaji na matengenezo ya baiskeli.

16. Fafanua hatua sita za uandaaji wa mlo kamili wenye uwiano wa virutubisho.

17. Changanua aina tano za majaribio yanayoweza kutumika katika upimaji wa somo la Stadi za Kazi.

18. Bainisha kanuni tano za kuheshimu haki miliki katika fani ya muziki.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org